

## **Wazo la kibiblia: "Nuru ya mchana" (2d edition)**



Unafikiri Nini ? Je, jua linatokea ao litoweka kwenye picha hii? Bila kujua majira, si rahisi kila mara kutambua wakati wa siku.

Katika hali kama na hiyo, wakati giza linapofunika maisha yetu, tunaweza kujiuliza ni nini hasa kinaendelea na nini cha kutarajia wakati ujao. Je, nuru itaendelea kungaa, kungaa zaidi, ao Mungu amelipitisha mbali nasi, kuzimika kabisa?

Hasa zaidi kwa wale wanao ishi Goma, Bukavu, miji na viji viyote Kongo Mashariki, na maeneo mengine mengi katika Kongo na Afrika ya Katanga, maisha yenu yamekuwa giza zaidi na ya kutisha. Wamoja wenu wamelazimika kukimbia nyumba zao. Wengine bado wangali mjini ao kijijini, lakini

muna wasiwasi kuhusu nini kinaweza kutokea baadaye. Wengine wenu wamekwama pale mulipo, mukijihisi pweke, mukivunjika moyo, na mukiwa na hofu, bila mahali pa kuenda. Pengine mambo yanaonekana kuwa kimia kwa sasa na munajitahidi muvezavyo kuendelea, lakini kivuli kiko kila mahali munakotazama.

Si rahisi kuishi chini ya kivuli cha uovu au kutokuwa na uhakika. Na hakuna mtu anayeweza kukuahidi kwamba mambo yatakuwa bora hapo karibuni. Lakini ninaweza kukuelekeza kwa yule anayefanya nuru ingae maishani mwangu, hasa ninapohisi kulemewa, kuvunjika moyo, ao hofu. Mtume Yoane aliandika juu yake katika Biblia, aliposema, "Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu wote. Nayo nuru yangaa gizani, wala giza halikuiweza" (Yohana 1:4-5, NRSV).

Yoane alikuwa akisema, Yesu Kristo alikuja katika ulimwengu huu kuangaza nuru ya Mungu katika giza lako. haijalishi kuonekana kinyume yako nyakati fulani, Muumba wako ni mzuri na anakujali. Bila kujali hali yako ya giza ao kutokuwa na upendo kwa wale walio karibu nawe kunaweza kuwa, ndani ya Yesu, kuna nuru. Kuna upendo. Na kuna tumaini kwako.

Jambo la maana ni kujua mahali pa kutafuta nuru na jinsi ya kuacha nuru ya Yesu iangaze zaidi katika moyo na akili yako. Unapashwa kuendeleza uhusiano wako na Mungu. Hakuna anayeweza kukufanya hivyo. Katika uzoefu wangu, ikiwa nataka zaidi ya Mungu, lazima nimufikie na kuweka macho yangu kwa Yesu. Lazima nijizungushe na wengine amba wanawenza kunitia moyo kwa uzoefu wao na Mungu, ndugu na dada zangu katika Kristo amba wanankumbusha kwamba siko peke yangu na kwamba Mungu anajibu maombi. Na kisha kinachonisaidia zaidi ni kutazama kando yangu, na kufanya kitu kwa ajili ya mtu mwingine. Ninaposaidia mizigo ya wengine na kuwatia moyo katika taabu zao, ninajisikia vizuri zaidi. Ninakusudia kuwa njia ya upendo wa Mungu kwao, kwa mwisho naona upendo wa Mungu kwangu katika mchakato huo. Na nuru katika maisha yangu inazidi kungaa.

Haijalishi ni nini unaweza kuwa unapitia maishani mwako, Yesu na awe Nuru ya siku yako leo na aangaze zaidi na zaidi katika moyo na akili yako katika siku zijazo.

Kwa upendo wa Yesu Kristo,

Professor et Pasteur Tim

Photo: Jua Linachomoka pa Chiang Mai, Thailand.

Tim Geoffrion ni mchungaji wa zamani ambaye amekuwa akiongoza Faith, Hope, and Love Global Ministries ([www.fhlglobal.org](http://www.fhlglobal.org)) kwa miaka 17. Anafundisha wanafunzi wa seminari, mapasta, na wizara zingine namna ya kujua, kupenda, na kutumikiya Mungu kwa ufanasi zaidi kama waongozi wanao ongozwa na Roho.